

KATIBU MKUU KIONGOZI, BALOZI HUSSEIN A. KATTANGA ATEMBELEA
BANDARI YA DAR ES SALAAM - 03/11/2021

Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Hussein A. Kattanga leo tarehe 3/11/2021 amefanya ziara ya kikazi katika Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania ambapo alikutana na menejimenti na baadhi ya wadau wa bandari na kukagua maeneo mbalimbali ya Bandari ya Dar es Salaam.

Katika ziara hiyo Katibu Mkuu Kiongozi aliambatana na Waratibu katika ofisi yake pamoja na Maafisa Waandamizi kutoka Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.

Mara baada ya kuwasili katika ofisi za mamlaka hiyo, Balozi Kattanga alifanya kikao kazi na uongozi wa mamlaka hiyo pamoja na baadhi ya Makatibu Wakuu, baadhi ya Wakuu wa Taasisi na baadhi ya maafisa waandamizi wa Serikali ambao ni wadau muhimu katika shughuli za kila siku za bandari. Makatibu Wakuu waliohudhuria kikao hicho ni Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Joseph Sokoine, Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Ndg. Dotto James na Kaimu Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ambaye alimwakilisha Katibu Mkuu.

Akiwasilisha taarifa ya utendaji, mkurugenzi mkuu wa mamlaka hiyo Ndg. Eric Benedict Hamissi alimweleza Katibu Mkuu Kiongozi hali ilivyo sasa ya kiutendaji katika Bandari zinazosimamiwa na Mamlaka hiyo nchini, ambapo kwa sasa bandari zote kuu nchini zina uwezo wa kuhudumia kiasi cha Tani milioni 20.4 za shehena mbalimbali kwa mwaka.

Aidha, alieleza kuwa, Bandari za Tanzania zinahudumia soko la ndani pamoja na la nchi za DR Congo, Rwanda, Burundi, Zambia, Malawi na Uganda, na uwezo wa kutoa huduma katika bandari hizo umeimarika katika kipindi cha miezi sita kuanzia Aprili hadi Septemba 2021 ukilinganisha na kipindi kama hicho kwa mwaka 2020. Katika kipindi hicho, jumla ya tani 9,230,944 za shehena za mizigo mbalimbali zimehudumiwa ikilinganishwa na tani 7,905,923 kwa mwaka 2020, ambapo ni ongezeko la asilimia 16.8, jumla ya meli 2,277 zimehudumiwa ikilinganishwa meli 1905 kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2020, hilo likiwa ongezeko la asilimia 17.8, jumla ya makasha (makontena) 390,263 yalihudumiwa ikilinganishwa na makasha 340,525 kwa kipindi hicho kwa mwaka 2020 hilo likiwa ni ongezeko la asilimia 14.6 na idadi ya magari yaliyohudumiwa katika bandari hizo hasa ya Dar es Salaam ni 74,512 ikilinganishwa magari 64,240 yaliyohudumiwa katika kipindi hicho kwa mwaka 2020 likiwa ni ongezeko la asilimia 16.

Pamoja na mafanikio hayo Mkurugenzi huyo alibainisha changamoto mbalimbali za kiutendaji zinazoikabili Mamlaka hiyo. Baadhi ya changamoto hizo ni ushindani kutoka bandari za nchi jirani za Afrika ya Mashariki na Kusini, ubovu wa miundombinu wezeshi kama vile barabara na reli katika nchi ambazo ni masoko ya huduma za Mamlaka hiyo pamoja na mikakati ya kibiashara inayofanywa nchi zenye bandari shindani.

Akipokea taarifa hiyo Katibu Mkuu Kiongozi aliwataka watendaji wa mamlaka hiyo kufikiria ni jinsi gani wataweza kushindana na washindani wao kimasoko ikiwa ni pamoja na kutatua kero zote zinazowakabili wateja wao ili kujenga imani kwao na kurudi kutumia bandari zetu. ***“Serikali imewekeza kwenye miradi wezeshi ya ujenzi wa barabara za lami, ujenzi wa reli ya kisasa, ujenzi wa bandari kavu na miradi mikubwa ya uzalishaji nishati ya umeme ili kuwezesha taasisi zake za kisekta ikiwemo Mamlaka ya Bandari kufanya kazi kiufanisi zaidi, hivyo TPA haina budi kujipanga kuingia katika ushindani mkubwa ili kushinda soko hasa la nchi jirani”***, alisistiza Katibu Mkuu Kiongozi.

Baada ya kikao hicho Katibu Mkuu Kiongozi pamoja na wajumbe walitembelea maeneo mbalimbali katika bandari ya Dar es Salaam kujionea hali halisi ya kiutendaji bandarini hapo. Maeneo aliyotembelea ni gati ya Malindi na kushuhudia meli ya ***Glovis*** ambayo ilikuwa inajiandaa kushusha shehena ya magari. Katibu Mkuu Kiongozi alitembelea pia sehemu ya upakuaji wa makontena pamoja na mizigo mingine, mizani wa Kurasini ya upimaji uzito wa mizigo iliyopakiwa katika malori yanayochukua mizigo kutoka bandarini hapo na mwisho alitembelea eneo maalum la upakuaji wa mafuta kutoka kwenye meli ***“Kurasini Oil Jetty” (KOJ)***.

Akihitimisha ziara yake hiyo, Katibu Mkuu Kiongozi alitoa rai kwa viongozi wa Mamlaka hiyo pamoja na wale wa wizara na taasisi za Serikali ambazo ni wadau wezeshi wa Mamlaka hiyo kufanya kazi kwa pamoja ili kuweza kutatua changamoto zinazoikabili Mamlaka hiyo.